Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

# Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano

Robo ya mwaka inayoishia Juni 2025

www.tcra.go.tz

VIWANGO VYA ISO 9001: 2015

Toleo 1.0

## Kuhusu ripoti hii

Ripoti hii inawasilisha takwimu za mawasiliano za robo ya nne ya mwaka wa fedha 2024/2025. Ripoti inatoa takwimu za mawasiliano ya simu, pesa mtandao kupitia simu za mkononi, intaneti, utangazaji, posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto.

Takwimu zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) vya kukusanya na kuandaa takwimu za huduma ya mawasiliano/TEHAMA.

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| **1** | **Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti** | **1** |
| 1.1 | Idadi ya laini za simu | 2 |
| 1.2 | Bei za huduma ya mawasiliano ya simu | 6 |
| 1.3 | Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu | 10 |
| 1.4 | Kuzuru | 17 |
| 1.5 | Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu | 18 |
| 1.6 | Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu | 19 |
| 1.7 | Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu | 20 |
| 1.8 | Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano | 21 |
| 1.9 | Huduma za intaneti | 22 |
| 1.10 | Huduma za pesa mtandao | 29 |
| 1.11 | Ubora wa huduma za simu na intaneti | 31 |
| 1.12 | Majaribio ya ulaghai | 37 |
| 1.13 | Leseni za huduma ya mawasiliano ya simu na intaneti | 40 |
| 1.14 | Vyeti | 40 |
| **2** | **Huduma za Utangazaji** | **42** |
| 2.1 | Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu | 42 |
| 2.2 | Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya | 43 |
| 2.3 | Ueneaji wa huduma za utangazaji | 45 |
| 2.4 | Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji | 45 |
| 2.5 | Leseni za huduma ya utangazaji | 48 |
| **3** | **Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto** | **50** |
| 3.1 | Idadi ya masanduku ya posta | 50 |
| 3.2 | Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 50 |
| 3.3 | Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa | 50 |
| 3.4 | Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa | 52 |
| 3.5 | Ubora wa huduma za Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 53 |
| 3.6 | Leseni za huduma ya Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 54 |
| **4** | **Hitimisho** | **55** |

# Muhtasari wa takwimu za Sekta ya Mawasiliano

**Idadi ya laini za simu**

**92.7 M**

136%

**Utumiaji wa intaneti**

**54.1 M**

79%

Upenyo

**Idadi ya dakika ndani ya nchi**

**43.3 B**

**Idadi ya dakika kutoka nje ya nchi**

**39.8 M**

**Matumizi ya intaneti**

**633 PB**

**Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa**

**2.0 M**

**17.6 K**

**Televisheni kwa njia ya waya**

**Bidhaa zilizotumwa**

559,529 — 61,602

**Bidhaa zilizopokelewa**

954,732 — 76,784

**Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya intaneti ya kasi**

3G **93%**

4G **92%**

5G **26%**

**Simu Janja**

**25 M**

37%

Upenyo

# Sura ya kwanza

## Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti



# 1. Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti

Sehemu hii inawasilisha takwimu za laini ya simu, bei, idadi ya dakika, ujumbe mfupi wa maneno (SMS), huduma ya intaneti, miundombinu na vifaa vya mawasiliano, upatikanaji wa huduma, ubora wa huduma na idadi ya watoa huduma.

## 1.1. Idadi ya laini za simu

Sehemu hii inawasilisha idadi ya laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zilitumika kwenye huduma ya mawasiliano angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kuna aina mbili za laini zinazotumika kwa mawasiliano, baina ya binadamu (Person to Person - P2P) na zinazotumika kwa mawasiliano ya vifaa na mitambo (Machine to Machine - M2M).

Jumla ya idadi ya laini (P2P na M2M) zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 90.4 katika robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025 hadi milioni 92.7 kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2025, hilo ni ongezeko la asilimia 2.6% kama inavyoonekana hapo chini.

**Kufikia Machi 2025**
**Milioni 90.4**

**Kufikia Juni 2025**
**Milioni 92.7**

**2.6%**

Jedwali 1.1 linaonesha idadi ya laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa kipindi kinachoishia Juni 2025.

**Jedwali 1.1 Idadi ya laini za simu za mkononi (P2P na M2M) na mezani**

| Mwezi | Simu za mkononi | Simu za mezani | Jumla |
|---|---|---|---|
| Aprili | 89,145,691 | 78,719 | 89,224,410 |
| Mei | 90,650,353 | 79,774 | 90,730,127 |
| Juni | 92,656,179 | 79,619 | 92,735,798 |

Laini za simu zimegawanywa kwa matumizi ya watu na mashine.

### 1.1.1 Idadi ya laini za P2P

**Kielelezo 1.1.1 Idadi ya laini za P2P**

Mpaka kufikia Juni 2025
**Milioni 91.7**

**Milioni 89.3**
Mpaka kufikia Machi 2025

**2.6%**

Laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa ajili ya P2P zimeongezeka kwa takribani milioni 2.3 katika robo mwaka inayoishia Juni 2025

Idadi ya laini za simu kwa matumizi ya watu kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.1.1.

**Jedwali 1.1.1 Idadi ya laini za simu za P2P zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 20,322,140 | 13,669,464 | 24,646,337 | 1,643,019 | 27,882,187 | 88,163,147 |
| Mei | 20,288,906 | 14,071,466 | 25,526,729 | 1,661,697 | 28,108,722 | 89,657,520 |
| Juni | 20,437,692 | 14,363,854 | 25,987,528 | 1,682,212 | 29,181,157 | 91,652,443 |

## 1.1.2 Idadi ya laini za simu kwa ajili ya vifaa (M2M)

**Kielelezo 1.1.2 Idadi ya laini za M2M**

Laini zilizosajiliwa kwa ajili ya mawasiliano ya M2M zimeongezeka kwa laini 33,078 kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025

**Mpaka kufikia Juni 2025**

**Milioni 1.08**

**Milioni 1.05**

**Mpaka kufikia Machi 2025**

**3.1%**

Jedwali 1.12 linaonesha idadi ya laini za simu kwa ajili ya matumizi ya vifaa kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025.

**Jedwali 1.1.2 Idadi ya laini za M2M zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 346,113 | 77,687 | 58,409 | 4,510 | 574,544 | 1,061,263 |
| Mei | 348,872 | 77,487 | 60,541 | 4,504 | 581,203 | 1,072,607 |
| Junii | 350,749 | 78,687 | 61,370 | 4,501 | 588,048 | 1,083,355 |

## 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma


Jedwali 1.1.3 inaonesha mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma.

**Jedwali 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma**

| Mwezi | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 20,668,253 | 13,747,151 | 24,704,746 | 1,647,529 | 28,456,731 | 89,224,410 |
| Mei | 20,637,778 | 14,148,953 | 25,587,270 | 1,666,201 | 28,689,925 | 90,730,127 |
| Juni | 20,788,441 | 14,442,541 | 26,048,898 | 1,686,713 | 29,769,205 | 92,735,798 |

Vodacom inaongoza kwenye soko kwa kuwa na 32.1% ikifuatiwa na Yas 28.1% na Airtel 22.4% kama inavyooneshwa kwenye chati 1.1.3.

**Chati 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma**





## 1.1.4 Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa na jinsia

**Kielelezo 1.1.4 Idadi ya laini za simu (P2P) kwa kila jinsia**




Katika robo ya nne ya mwaka 2024/2025 Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 17.07, Mwanza ilishika nafasi ya pili kwa kuwa na laini milioni 6.14, Arusha ilishika nafasi ya tatu kwa kuwa na laini milioni 5.58, Mbeya ilishika nafasi ya nne ikiwa na laini milioni 5.34, na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 4.95. Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye ramani 1.1.4.

**Ramani 1.1.4 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa kila mkoa**




## 1.1.5 Mwenendo wa idadi ya laini za simu

Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa ajili ya mawasiliano ya simu kwa robo mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita imeoneshwa katika Jedwali 1.1.5a na 1.1.5b.

**Jedwali 1.1.5a Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Laini za simu za mkononi | 80,583,993 | 86,769,161 | 90,298,941 | 92,656,179 |
| Laini za simu za mezani | 78,048 | 78,299 | 79,054 | 79,619 |
| **Jumla** | **80,662,041** | **86,847,460** | **90,377,995** | **92,735,798** |
| **Asilimia ya Ueneaji** | **124.0%** | **133.5%** | **132.6%** | **136.1%** |

**Jedwali 1.1.5b Idadi ya laini za simu kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Simu za mkononi | 51,220,233 | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 | 86,769,161 |
| Simu za mezani | 72,469 | 71,834 | 84,696 | 75,732 | 78,299 |
| **Jumla** | **51,292,702** | **54,118,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | **86,847,460** |
| **Asilimia ya Ueneaji** | **81.0%** | **88.0%** | **98.0%** | **111.0%** | **133.5%** |

## 1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

Sehemu hii inawasilisha wastani wa bei ndani na nje ya vifurushi (pamoja na kodi) kwa huduma za sauti, SMS, na data kwa matumizi ya ndani na nje ya mtandao, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu nje ya kifurushi

Hizi ni bei zinazotozwa kwa huduma za sauti kwa dakika, SMS, na data kwa MB bila kujiunga katika kifurushi.

**Kielelezo 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu**

| | Machi 2025 | Juni 2025 | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 26.00 | 26.00 | 0% |
| Nje ya mtandao | 28.00 | 28.00 | 0% |
| SMS Kitaifa | 7.80 | 7.80 | 0% |
| SMS Kimataifa | 189.60 | 189.60 | 0% |
| Afrika Mashariki | 627.80 | 247.52 | -61% |
| Mataifa mengine | 1,935.00 | 2,175.15 | 12% |
| Data | 9.35 | 9.35 | 0% |

Kama inavyooneshwa katika muhtasari hapo juu, wakati bei za kupiga simu ndani na nje ya mtandao, SMS kitaifa, SMS kimataifa na data hazikubadilika, bei za kupiga simu za Afrika Mashariki imepungua kwa 61% na mataifa mengine iliongezeka kwa 12%. Bei za huduma za sauti za EA kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025 zimezingatia gharama za makubaliano ya kikanda (EAC harmonised roaming framework).

### 1.2.1.1 Bei za huduma ya sauti (Tsh)

Bei za huduma ya sauti kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2025 kwa simu za ndani na nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.1. Hizi ni bei za sauti kwa dakika moja kwa kupiga simu ya ndani au ya kimataifa bila kujiunga kwenye kifurushi.

**Jedwali 1.2.1.1 Bei (Tsh) za kupiga simu ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma**

| Mtoa huduma | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | Afrika Mashariki | Mataifa mengine |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 30.00 | 30.00 | 260.00 | 2,050.00 |
| Halotel | 10.00 | 20.00 | 250.00 | 1,424.44 |
| Yas | 30.00 | 30.00 | 260.00 | 1,846.67 |
| TTCL | 30.00 | 30.00 | 217.60 | 2,871.33 |
| Vodacom | 30.00 | 30.00 | 250.00 | 2,383.33 |
| **Wastani** | 26.00 | 28.00 | 247.52 | 2,175.15 |

Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa watoa huduma wote walitoza Tsh 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, isipokuwa Halotel alitoza Tsh 10 kwa dakika ndani ya mtandao na Tsh 20 nje ya mtandao.

Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani ya mtandao katika robo mwaka inayoishia Juni 2025 ilibaki Tsh 26 na Tsh 28 kwa dakika ndani na nje ya mtandao mtawalia sawa na robo mwaka iliyoishia Machi 2025.

Aidha, Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa bei ya huduma ya sauti kimataifa zilitofautiana baina ya watoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti kwa dakika moja kwa Afrika Mashariki na nchi nyingine ni Tsh 247.52 na 2,175.15 mtawalia.

### 1.2.1.2 Bei za SMS na data (Tsh)

Bei bila kifurushi nje na ndani ya nchi kwa SMS na data hadi Juni 2025 zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.2.

**Jedwali 1.2.1.2 Bei (Tsh) za SMS na data**

| Mtoa huduma | SMS ndani ya nchi | SMS nje ya nchi | Data/Mb |
|---|---|---|---|
| Airtel | 8.00 | 215.00 | 9.35 |
| Halotel | 5.00 | 95.00 | 9.35 |
| Yas | 8.00 | 215.00 | 9.35 |
| TTCL | 10.00 | 138.00 | 9.35 |
| Vodacom | 8.00 | 285.00 | 9.35 |
| Wastani | 7.80 | 189.60 | 9.35 |

Wastani wa bei za SMS kitaifa (Tsh 7.80), SMS nje ya nchi (Tsh 189.60) na data (Tsh 9.35) kwa Juni 2025 ulibaki kama ilivyokuwa kwenye robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025.

### 1.2.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa dakika moja ya sauti, SMS moja na MB moja ya data kwa watumiaji waliojiunga na kifurushi zimeoneshwa kwenye jedwali 1.2.2a.

**Jedwali 1.2.2a Mabadiliko ya bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi**

| Kipindi | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Juni 2025 | 4.80 | 5.96 | 1.52 | 2.12 |
| Machi 2025 | 4.80 | 6.07 | 1.55 | 2.12 |
| Badiliko % | 0.00% | -1.92% | -2.06% | 0.00% |

Jedwali 1.2.2a linaonesha kuwa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi zimebadilika katika robo ya mwaka inayoishia Juni 2025 ikilinganishwa na robo ya mwaka inayoishia Machi 2025. Bei za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao, na SMS ziliongezeka kwa viwango tofauti kama ilivyooneshwa.

Jedwali 1.2.2b linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika kifurushi ziko chini ikilinganishwa na bei za huduma za mawasiliano ya simu bila kifurushi.

**Jedwali 1.2.2b Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi**

| Mtoa huduma | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 4.39 | 7.62 | 11.68 | 2.05 |
| Halotel | 3.02 | 4.76 | 1.00 | 2.16 |
| Yas | 5.40 | 4.80 | 0.80 | 2.05 |
| TTCL | 6.80 | 6.80 | 2.07 | 2.08 |
| Vodacom | 4.39 | 5.80 | 2.07 | 2.28 |
| Wastani kwa Sekta | 4.80 | 5.96 | 1.52 | 2.12 |

### 1.2.3 Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya kifurushi kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.3.

**Jedwali 1.2.3 Wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu**

| | Ndani ya mtandao | Nje ya mtandao | SMS | Data |
|---|---|---|---|---|
| Wastani bila kifurushi | 26.00 | 28.00 | 7.80 | 9.35 |
| Wastani katika kifurushi | 4.80 | 5.96 | 1.52 | 2.12 |

Jedwali 1.2.3 linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu bila kifurushi ni zaidi ya wastani wa bei katika kifurushi na hivyo kupelekea watumiaji wengi (99.9%) kupendelea kujiunga na huduma za vifurushi.

### 1.2.4 Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za sauti na SMS nje ya vifurushi, kitaifa na kimataifa katika kipindi cha robo mwaka na miaka mitano imeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.4a, 1.2.4b, 1.2.4c, 1.2.4d, 1.2.4e, 1.2.4f, 1.2.4g na 1.2.4h.

**Jedwali 1.2.4a Mwenendo wa wastani wa bei ((Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 26.00 | 26.00 | 26.00 | 26.00 |
| Nje ya mtandao | 28.00 | 28.00 | 28.00 | 28.00 |

**Jedwali 1.2.4b Mwenendo wa wastani wa bei ((Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 57.00 | 34.00 | 32.00 | 29.00 | 26.00 |
| Nje ya mtandao | 57.00 | 34.00 | 32.00 | 30.00 | 28.00 |

**Jedwali 1.2.4c Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Afrika Mashariki | 696.68 | 597.40 | 627.80 | 247.52 |
| Mataifa mengine | 1,948.22 | 2,016.70 | 1,935.00 | 2,175.15 |

**Jedwali 1.2.4d Mwenendo wa wastani wa bei ((Tsh kwa dakika) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Afrika Mashariki | 830.00 | 966.00 | 1,103.00 | 1,171.00 | 684.00 |
| Mataifa mengine | 1,379.00 | 1,564.00 | 1,817.00 | 1,776.00 | 2,055.00 |

**Jedwali 1.2.4e Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| SMS kitaifa | 7.80 | 7.80 | 7.80 | 7.80 |
| SMS kimataifa | 189.60 | 189.60 | 189.60 | 189.60 |

**Jedwali 1.2.4f Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| SMS kitaifa | 20.00 | 13.00 | 11.00 | 11.00 | 7.80 |
| SMS kimataifa | 176.00 | 172.00 | 193.00 | 200.00 | 189.60 |

**Jedwali 1.2.4g Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 4.75 | 4.79 | 4.80 | 4.80 |
| Nje ya mtandao | 6.34 | 6.27 | 6.07 | 5.96 |
| SMS | 1.47 | 1.57 | 1.55 | 1.52 |
| Data | 2.17 | 2.16 | 2.12 | 2.12 |

**Jedwali 1.2.4h Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 9.38 | 7.84 | 7.27 | 4.90 | 4.68 |
| Nje ya mtandao | 11.21 | 8.69 | 7.78 | 6.30 | 6.22 |
| SMS | 3.45 | 3.35 | 2.69 | 1.37 | 1.46 |
| Data | 1.73 | 1.61 | 1.86 | 2.14 | 2.17 |

## 1.3 Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu

Sehemu hii inatoa mwenendo wa simu zilizopigwa ndani na nje ya nchi pamoja na ujumbe mfupi wa maneno

### 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti

#### 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi

Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini kwa robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025 na Juni 2025 imeoneshwa hapo chini.

| Kufikia Machi 2025 | Kufikia Juni 2025 | |
|---|---|---|
| **Bilioni 40.6** | **Bilioni 43.3** | **6.6%** |

Kielelezo hapo juu kinaonesha kuongezeka kwa idadi ya dakika za huduma za sauti ndani ya nchi kwa 6.6% katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025.

**Kielelezo 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi**

| | Robo mwaka iliyoishia Machi 2025 | Robo mwaka iliyoishia Juni 2025 | Mabadiliko |
|---|---|---|---|
| Ndani ya Mtandao | 20.2 Billion | 21.5 Billion | 6.3% |
| Nje ya Mtandao | 20.4 Billion | 21.8 Billion | 6.9% |

Jedwali 1.3.1.1 linaonesha kuwa Juni 2025 ulikuwa mwezi wenye idadi ya dakika nyingi zaidi ikilinganishwa na miezi mingine ya robo mwaka huo.


Jedwali 1.3.1 linaonesha dakika bilioni 43.3 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Juni 2025 ikilinganishwa na dakika bilioni 40.6 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2025. Katika kipindi hicho, idadi ya dakika nje ya mtandao ilikuwa kubwa zaidi ikilinganishwa na ndani ya mtandao katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025. Pia, mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka na miaka mitano unaoneshwa kwenye jedwali 1.3.1.1b na 1.3.1.1c.

**Jedwali 1.3.1.1a Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini**


| | Aprili | Mei | Juni | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 6,857,484,028 | 7,192,651,662 | 7,442,821,262 | **21,492,956,952** |
| Nje ya mtandao | 6,882,436,627 | 7,364,253,101 | 7,512,515,634 | **21,759,205,362** |
| **Jumla** | 13,739,920,655 | 14,556,904,763 | 14,955,336,896 | **43,252,162,314** |

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.1b na 1.3.1.1c. Airtel imeongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya dakika za ndani ya mtandao (35.1%) na nje ya mtandao (28.4%).

**Chati 1.3.1.1b Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani ya mtandao kwa kila mtoa huduma**




**Chati 1.3.1.1c Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti nje ya mtandao kwa kila mtoa huduma**




**Jedwali 1.3.1.1b Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka**


| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 21,088,541,912 | 20,990,181,336 | 20,223,164,062 | 21,492,956,952 |
| Nje ya mtandao | 20,033,335,066 | 21,487,957,832 | 20,345,309,688 | 21,759,205,362 |
| Jumla | 41,121,876,978 | 42,478,139,168 | 40,568,473,750 | 43,252,162,314 |

**Jedwali 1.3.1.1c Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 54,561,254,851 | 51,673,651,476 | 62,678,814,642 | 77,770,241,513 | 81,916,822,649 |
| Nje ya mtandao | 27,084,539,242 | 43,194,917,029 | 60,064,367,493 | 67,100,445,506 | 76,215,903,038 |
| Jumla | 81,645,794,093 | 94,868,568,505 | 122,743,182,135 | 144,870,687,019 | 158,132,725,687 |

## 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti nje ya nchi

Idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi imeoneshwa hapo chini.




Kielelezo kinaonesha kuongezeka kwa idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025. Idadi ya dakika kwenda nje ya nchi imeongezeka kwa 20%. Kwa upande mwingine, dakika kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa 10%. Vilevile, takwimu zinaonesha kulikuwa na idadi kubwa ya dakika kwenda nje ya nchi ikilinganishwa na zilizotoka nje ya nchi.


Jumla ya dakika kwenda na kutoka Afrika Mashariki (EA) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na mataifa mengine (RoW) kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa katika Jedwali 1.3.1.2a.

**Jedwali 1.3.1.2a Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025**


| | Aprili | Mei | Juni | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 50,126,613 | 53,913,461 | 52,873,867 | **156,913,941** |
| Kutoka EA | 11,082,820 | 11,676,979 | 12,001,259 | **34,761,058** |
| Kwenda SADC | 94,527 | 119,174 | 96,905 | **310,606** |
| Kutoka SADC | 208,727 | 377,331 | 249,592 | **835,650** |
| Kwenda RoW | 735,574 | 727,968 | 761,322 | **2,224,864** |
| Kutoka RoW | 1,289,112 | 1,475,819 | 1,390,204 | **4,155,135** |

Mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka EA, SADC na Mataifa Mengine (RoW) umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.2a , Chati 1.3.1.2b na Chati 1.3.1.2c


**Chati 1.3.1.2a Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA**




**Chati 1.3.1.2b Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka SADC**




**Chati 1.3.1.2c Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW**




**Jedwali 1.3.1.2b Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 101,188,767 | 124,483,791 | 129,398,936 | 156,913,941 |
| Kutoka EA | 26,794,839 | 30,688,068 | 31,009,232 | 34,761,058 |
| Kwenda SADC | 385,614 | 328,305 | 281,939 | 310,606 |
| Kutoka SADC | 760,089 | 754,317 | 591,422 | 835,650 |
| Kwenda RoW | 10,900,864 | 5,276,392 | 3,715,324 | 2,224,864 |
| Kutoka RoW | 6,032,139 | 6,642,832 | 5,023,166 | 4,155,135 |

**Jedwali 1.3.1.2c Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 9,738,521 | 9,097,165 | 8,927,113 | 95,473,684 | 363,293,881 |
| Kutoka EA | 15,406,649 | 15,853,362 | 13,594,473 | 34,994,641 | 108,663,455 |
| Kwenda RoW | 38,014,133 | 24,856,947 | 26,034,131 | 19,510,999 | 36,294,294 |
| Kutoka RoW | 45,172,263 | 49,885,142 | 33,374,619 | 23,681,940 | 24,858,074 |

## 1.3.2 Idadi ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

### 1.3.2.1 Idadi ya SMS ndani ya nchi

Kielelezo kinaonesha idadi ya SMS imeongezeka kwa 6% kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2025.

| Robo mwaka inayoishia Machi 2025 | Robo mwaka inayoishia Juni 2025 | |
|---|---|---|
| **Bilioni 50.0** | **Bilioni 52.8** | **6%** |

| Robo mwaka | SMS ndani ya mtandao | SMS nje ya mtandao | Jumla |
|---|---|---|---|
| Machi 2025 | Bilioni 21.1 | Bilioni 28.9 | Bilioni 50.0 |
| Juni 2025 | Bilioni 22.3 | Bilioni 30.5 | Bilioni 52.8 |
| **Badiliko** | **6%** | **5%** | **6%** |

Jedwali 1.3.2.1a linaonesha mabadiliko ya idadi ya SMS ndani na nje ya mtandao. Mwezi Juni 2025 ulikuwa na idadi kubwa ya SMS ikilinganishwa na miezi mingine kwenye kipindi husika.

**Jedwali 1.3.2.1a Idadi ya SMS ndani ya nchi**

| | Aprili | Mei | Juni | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 7,424,445,399 | 7,323,523,648 | 7,553,431,197 | **22,301,400,244** |
| Nje ya mtandao | 10,101,481,970 | 10,019,896,806 | 10,394,691,630 | **30,516,070,406** |
| Jumla | 17,525,927,369 | 17,343,420,454 | 17,948,122,827 | **52,817,470,650** |

Mwenendo wa idadi ya SMS ndani ya nchi imeoneshwa katika jedwali 1.3.2.1b na 1.3.2.1c.

**Jedwali 1.3.2.1b Mwenendo wa idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 20,222,806,831 | 22,246,288,233 | 21,081,683,531 | 22,301,400,244 |
| Nje ya mtandao | 27,374,852,630 | 30,644,175,708 | 28,937,308,450 | 30,516,070,406 |
| Jumla | 47,567,659,461 | 52,890,463,941 | 50,018,991,981 | 52,817,470,650 |

### Jedwali 1.3.2.1c Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ndani ya mtandao | 61,971,569,487 | 58,875,779,663 | 65,358,270,089 | 84,818,793,761 | 84,909,556,665 |
| Nje ya mtandao | 71,072,186,913 | 78,200,512,436 | 88,154,239,625 | 121,727,776,013 | 116,828,465,147 |
| Jumla | 133,043,756,400 | 137,076,292,099 | 153,512,509,714 | 206,546,569,774 | 201,738,021,812 |

## 1.3.2.2 Idadi ya SMS kutoka na kwenda nje ya nchi


Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW imeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2a.

### Jedwali 1.3.2.2a Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW


| | Aprili | Mei | Juni | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 143,467 | 1141,812 | 142,475 | **427,754** |
| Kutoka EA | 3,770,431 | 3,166,427 | 3,558,822 | **10,495,680** |
| Kwenda SADC | 27,534 | 27,724 | 30,585 | **85,843** |
| Kutoka SADC | 321,912 | 312,054 | 318,459 | **952,425** |
| Kwenda RoW | 343,349 | 366,089 | 418,854 | **1,128,292** |
| Kutoka RoW | 694,589,237 | 757,065,392 | 666,663,720 | **2,118,318,349** |

Jedwali 1.3.3.2a linaonesha kuwa idadi kubwa ya SMS zilipokelewa kutoka EA, SADC na RoW kuliko zilizotumwa EA, SADC na RoW. Uwiano wa SMS zilizotumwa na kupokelewa imeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.2a, 1.3.2.2b na 1.3.2.2c.


### Chati 1.3.2.2a Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka EA




### Chati 1.3.2.2b Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka SADC



## Chati 1.3.2.2c Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka RoW




Mwenendo wa idadi ya SMS EA, SADC na RoW kwa robo mwaka na kipindi cha miaka mitano inaoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2b na 1.3.2.2c.

### Jedwali 1.3.2.2b Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA, SADC na RoW kwa robo mwaka

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 477,221 | 494,451 | 435,676 | 427,754 |
| Kutoka EA | 8,083,034 | 8,147,519 | 7,835,696 | 10,495,680 |
| Kwenda SADC | 194,337 | 105,338 | 89,400 | 85,843 |
| Kutoka SADC | 1,146,923 | 1,531,911 | 1,033,306 | 952,425 |
| Kwenda RoW | 1,131,776 | 1,531,911 | 1,256,169 | 1,128,292 |
| Kutoka RoW | 1,365,055,223 | 1,548,631,201 | 1,785,739,892 | 2,118,318,349 |

### Jedwali 1.3.2.2c Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda EA | 1,235,692 | 1,425,624 | 1,700,525 | 2,233,288 | 1,896,295 |
| Kutoka EA | 50,880,982 | 89,717,530 | 58,344,672 | 37,592,410 | 41,662,728 |
| Kwenda RoW | 2,718,443 | 3,191,041 | 3,574,956 | 5,448,764 | 13,342,306 |
| Kutoka RoW | 3,935,379,714 | 4,599,468,894 | 4,664,200,079 | 5,562,047,440 | 5,798,188,788 |

## 1.4 Kuzuru

Sehemu hii inaonesha idadi ya dakika ya huduma ya sauti, SMS na Data kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru (roaming) kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025.

**Kielelezo 1.4 Kuzuru**

| | Dakika | SMS | Data |
|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | Bilioni 8.05 | Milioni 11.54 | 5,972 PB |
| Kuzuru Kutoka | Bilioni 0.82 | Milioni 9.05 | 157,279 PB |

### 1.4.1 Kuzuru huduma ya sauti (dakika)

Idadi ya dakika kwa huduma ya kuzuru ya sauti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.1.

**Jedwali 1.4.1 Kuzuru huduma ya sauti (dakika)**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 13,620,217 | 34,585 | 8,038,960,081 | 8,052,614,883 |
| Kuzuru Kutoka | 669,379,449 | 4,705,185 | 145,342,427 | 819,427,061 |

### 1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS

Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.2.

**Jedwali 1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 4,118,782 | 316,106 | 7,104,495 | 11,539,383 |
| Kuzuru Kutoka | 6,128,638 | 798,783 | 2,117,793 | 9,045,214 |

### 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti

Idadi ya megabaiti kutoka na kwenda EA, SADC na RoW kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.3.


**Jedwali 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti (megabytes)**

| | EA | SADC | RoW | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kuzuru kwenda | 2,080,795 | 868,838 | 5,972,835,691,294 | 5,972,838,640,927 |
| Kuzuru Kutoka | 4,337,601,288,203 | 5,660,659,934,054 | 147,281,230,242,922 | 157,279,491,465,179 |

## 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu

Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini ya simu ndiyo kichocheo kikubwa katika kukuza matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu/TEHAMA nchini. Idadi ya vifaa vilivyounganishwa kwenye mitandao ya simu imeoneshwa kwenye Jedwali 1.5.

**Kielelezo 1.5 Upenyo wa simu za mkononi**




Kufikia Juni 2025, asilimia ya simu janja (smartphones) kwa idadi ya watu imeongezeka kufikia 36.75% kutoka 35.29% katika mwezi Machi 2025. Aidha, asilimia ya simu za rununu (feature phones) imeongezeka kutoka 82.64% mwezi Machi 2025 na kufikia 84.97% mwezi Juni 2025. Ueneaji wa vifaa vingine vya mawasiliano miongoni mwa watu ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.5.


**Jedwali 1.5. Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu na kuunganishwa kwenye mtandao**

| Aina ya kifaa | Idadi ya Vifaa | Upenyo (Penetration) |
|---|---|---|
| Simu za rununu (Feature phones) | 57,911,926 | 84.97% |
| Simu janja (Smartphones) | 25,048,038 | 36.75% |
| Handheld | 1,584,279 | 2.32% |
| Modem | 712,857 | 1.05% |
| Tablet | 552,358 | 0.81% |
| WLAN Router | 280,067 | 0.41% |
| IoT Device | 160,984 | 0.24% |
| Dongle | 89,104 | 0.13% |
| Module | 74,655 | 0.11% |
| Portable(include PDA) | 48,566 | 0.07% |
| Connected Computer | 13,092 | 0.02% |
| Vehicle | 9,154 | 0.01% |
| Wearable | 9,060 | 0.01% |
| Device for the Automatic Processing of Data (APD) | 4,083 | 0.01% |

## 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu

Hadi kufikia Juni 2025, idadi ya minara ya huduma ya mawasiliano ya simu ilikuwa ni 9,448. Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya minara 1,222. Mgawanyo wa idadi ya minara kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye ramani 1.6.

### Ramani 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu




## 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu

Jedwali 1.7 linaonesha idadi ya mitambo ya 2G, 3G, 4G na 5G kwa kila mkoa hadi kufikia Juni 2025.

### Jedwali 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu kimkoa

| Mkoa | Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi | | | |
|---|---|---|---|---|
| | BTS (2G) | NodeB (3G) | eNB (4G) | gNB (5G) |
| **Tanzania Bara** | | | | |
| Arusha | 726 | 693 | 691 | 37 |
| Dar-es-salaam | 2390 | 2469 | 2479 | 688 |
| Dodoma | 723 | 604 | 644 | 50 |
| Geita | 409 | 391 | 378 | 8 |
| Iringa | 414 | 366 | 378 | 6 |
| Kagera | 538 | 509 | 483 | 2 |
| Katavi | 176 | 154 | 157 | 2 |
| Kigoma | 487 | 439 | 421 | 5 |
| Kilimanjaro | 570 | 538 | 540 | 11 |
| Lindi | 354 | 271 | 295 | 3 |
| Manyara | 367 | 301 | 313 | 1 |
| Mara | 428 | 388 | 389 | 5 |
| Mbeya | 593 | 571 | 581 | 19 |
| Morogoro | 740 | 649 | 675 | 13 |
| Mtwara | 434 | 361 | 374 | 2 |
| Mwanza | 769 | 745 | 739 | 46 |
| Njombe | 322 | 283 | 287 | 3 |
| Pwani | 545 | 472 | 515 | 13 |
| Rukwa | 291 | 259 | 251 | 1 |
| Ruvuma | 446 | 361 | 375 | 4 |
| Shinyanga | 397 | 377 | 362 | 6 |
| Simiyu | 303 | 267 | 261 | 2 |
| Singida | 363 | 330 | 327 | 4 |
| Songwe | 253 | 223 | 219 | 13 |
| Tabora | 555 | 497 | 451 | 6 |
| Tanga | 647 | 557 | 572 | 9 |
| **Zanzibar** | | | | |
| Kaskazini Pemba | 64 | 63 | 57 | 2 |
| Kaskazini Unguja | 88 | 88 | 87 | 4 |
| Kusini Pemba | 67 | 68 | 66 | 2 |
| Kusini Unguja | 107 | 103 | 106 | 6 |
| Mjini Magharibi | 246 | 260 | 263 | 65 |
| **Jumla** | **14,812** | **13,657** | **13,736** | **1,038** |

**Kielelezo 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi kwa teknolojia**




Jedwali 1.7 linaonesha kuenea kwa kiasi kikubwa kwa teknolojia ya 2G na 3G, ikiwa na BTS 14,812 na NodeB 13,657. Japokuwa teknolojia ya 4G haijaenea kama 2G na 3G, idadi ya eNB zimefika 13,736. Aidha, gNB zimeongezeka kwa kiasi cha asilimia 11 zikiwa zimefika 1,038 na zimeenea zaidi katika maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam na Mjini Magharibi. Hata hivyo, Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kwa teknolojia zote (2G, 3G, 4G na 5G), na kuifanya kuwa kitovu cha mawasiliano nchini.

## 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano

Uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano umeongeza usambaaji wa huduma ya mawasiliano kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.8.

**Jedwali 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano**

| | | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|
| Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya mawasiliano | 2G | 98.4% | 98.6% |
| | 3G | 92.2% | 93.4% |
| | 4G | 90.7% | 92.0% |
| | 5G | 23.0% | 26.0% |
| Asilimia ya eneo lilofikiwa na huduma ya mawasiliano | 2G | 76.2% | 77.4% |
| | 3G | 74.1% | 75.0% |
| | 4G | 73.6% | 75.0% |
| | 5G | 3.6% | 5.9% |

Jedwali 1.8, linaonesha kuenea kwa wigo wa mawasiliano 2G, 3G, 4G na 5G kufikia 98.6%, 93.4%, 92.0%, na 26.0% ya watu nchini, mtawalia. Aidha, asilimia ya eneo lilofikiwa na mawasiliano ya 2G, 3G, 4G na 5G ni 77.4%, 75.0%, 75.0%, na 5.9%, mtawalia.

## 1.9 Huduma za Intaneti

### 1.9.1 Utumiaji wa Intaneti

Huduma ya intaneti inatolewa kwa kutumia laini za simu, waya (faiba), na mawimbi (wireless). idadi ya utumiaji wa intaneti inatokana na laini/waya ambazo zimetumia huduma ya Intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika (FTTX, 2G - GPRS na EDGE, 3G, 4G, au 5G).

Utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye kielelezo hapo chini

| Kufikia Machi 2025 | Kufikia Juni 2025 | |
|---|---|---|
| **Milioni 49.3** | **Milioni 54.1** | **9.6%** |

Idadi ya utumiaji wa Intaneti imeongezeka kwa 9.6% kutoka milioni 49.3 kwa robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025 hadi milioni 54.1 kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025.

Idadi ya utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.9.1a. Jedwali hilo linaonesha kuwa huduma ya intaneti kwa njia ya simu ya mkononi inapendelewa zaidi (99.5%) ikilinganishwa na huduma ya intaneti isiyoashimishika.

**Jedwali 1.9.1a Idadi ya utumiaji wa Intaneti kufikia mwisho wa kila mwezi katika robo ya mwaka inayoishia Juni 2025**


| Mwezi | Mobile Wireless | Fixed Wireless | Fixed Wired | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Aprili | 52,186,717 | 153,484 | 92,999 | **52,433,200** |
| Mei | 52,839,236 | 154,080 | 97,146 | **53,090,462** |
| Juni | 53,815,513 | 164,945 | 98,072 | **54,078,530** |
| **Internet Penetration** | | | | **79.3%** |

Jedwali 1.9.1b linaonesha idadi ya utumiaji wa intaneti kwa teknolojia mbalimbali ikiwa kwa njia ya simu za mkononi au isiyohamishika (fixed). Kielelezo 1.9.1a kinaonesha kuwa intaneti ya kasi kwa huduma ya simu ndiyo njia inayopendelewa zaidi kupata intaneti, ikiwa na laini 30,232,986 . Teknolojia ya 2G bado ina matumizi makubwa, ikiwa na laini 23,582,527. Teknolojia za faiba Nyumbani (Fiber to the Home - FTTH) na faiba Ofisini (Fiber to the Office - FTTO) zina idadi ndogo ya laini 83,175 na 14,897 mtawalia.


## Jedwali 1.9.1b Idadi ya utumiaji wa intaneti kwa teknolojia

| Teknolojia | Aprili | Mei | Juni |
|---|---|---|---|
| 2G | 23,048,147 | 23,124,280 | 23,582,527 |
| 3G | 5,190,642 | 5,077,965 | 4,987,535 |
| 4G | 22,762,488 | 23,396,945 | 23,933,438 |
| 5G | 1,185,440 | 1,240,046 | 1,312,013 |
| FTTH | 78,890 | 83,474 | 83,175 |
| FTTO | 14,109 | 13,672 | 14,897 |
| Terrestrial fixed wireless | 146,552 | 147,200 | 158,048 |
| Setelaite | 1,351 | 1,372 | 1,390 |
| Teknolojia nyingine | 5,581 | 5,508 | 5,507 |
| **Jumla** | **52,433,200** | **53,090,462** | **54,078,530** |


**Kielelezo 1.9.1a Utumiaji wa intaneti kwa teknolojia**



## Chati 1.9.1a Mgawanyo wa huduma ya Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025




## Chati 1.9.1b Idadi ya laini za intaneti (fixed) kwa kila mtoa huduma





Usajili wa laini za intaneti (fixed) kwa watu binafsi ni **193,288**

Usajili wa laini za intaneti (fixed) kwa taasisi ni **69,729**

### Jedwali 1.9.1c Idadi ya usajili kwa kasi ya intaneti (Internet subscription by speed)


| Kasi | Idadi ya usajili |
|---|---|
| <256 Kbps | 7 |
| >= 256 Kbps< 2Mbps | 1,189 |
| >= 2Mbps< 10Mbps | 23,330 |
| >= 10Mbps< 100Mbps | 233,275 |
| >= 100Mbps< 1Gbps | 4,885 |
| >= 1Gbps | 331 |
| **Jumla** | **263,017** |

**Kielelezo 1.9.1b Idadi ya utumiaji wa huduma ya Intaneti kwa robo mwaka**





Kielelezo 1.9.1b inaonesha wastani wa ukuaji wa 9.5% ya idadi ya utumiaji wa huduma ya intaneti kutoka Septemba 2024 mpaka Juni 2025.

### Chati 1.9.1c Idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa miaka mitano iliyopita



## 1.9.2 Matumizi ya huduma ya Intaneti

Matumizi ya huduma ya Intaneti huhesabiwa kama kiasi cha data (katika Petabytes) kilichotumiwa katika kipindi husika. (1 Petabyte = $1000^3$ Megabytes).





**Jedwali 1.9.2 Kiasi cha data kilichotumika katika robo ya mwaka inayoishia Juni 2025**

| | Aprili | Mei | Juni |
|---|---|---|---|
| Kiasi cha data (GB) | 208,882,149 | 206,408,453 | 217,798,231 |
| usajili wa intaneti | 52,433,200 | 53,090,462 | 54,078,530 |
| GB kwa kila usajili | 3.98 | 3.89 | 4.03 |

Jedwali 1.9.2 linaonesha kuwa kila usajili wa intaneti ulitumia wastani wa GB 4.03 kwa mwezi Juni ambayo ni zaidi ikilinganishwa na Aprili na Mei.

## 1.9.3 Wastani wa kasi ya intaneti

**Kielelezo 1.9.3 Wastani wa kasi ya kupakua na kupakia**



**1.9.3a Kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti wa kupakua (Mbps) kwa maeneo yaliopimwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025**

| Mikoa | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 16.5 | 22.4 | 28.3 | 15.0 | 17.1 | 19.85 |
| Dodoma | 15.5 | 15.4 | 19.4 | 15.4 | 13.5 | 15.85 |
| Katavi | 7.9 | 14.4 | 23.4 | 23.1 | 19.7 | 17.67 |
| Kilimanjaro | 21.8 | 21.6 | 27.1 | 19.8 | 22.1 | 22.49 |
| Manyara | 17.4 | 20.4 | 19.8 | 20.0 | 17.3 | 18.97 |
| Mbeya | 18.6 | 19.1 | 25.8 | 24.9 | 13.5 | 20.35 |
| Mtwara | 15.1 | 20.7 | 27.1 | 23.7 | 21.3 | 21.57 |
| Mwanza | 24.7 | 18.4 | 22.3 | 23.8 | 14.8 | 20.81 |
| Pemba | 9.0 | 14.4 | 24.6 | 12.5 | 20.4 | 16.18 |
| Rukwa | 10.8 | 17.3 | 25.7 | 23.8 | 17.8 | 19.08 |
| Singida | 15.8 | 18.1 | 25.0 | 18.4 | 23.3 | 20.14 |
| Songwe | 21.3 | 15.6 | 21.7 | 20.4 | 9.5 | 17.71 |
| Tabora | 20.7 | 19.5 | 21.9 | 22.2 | 18.3 | 20.51 |
| Unguja | 13.5 | 18.7 | 23.2 | 20.3 | 27.4 | 20.60 |
| **Wastani wa sekta** | | | | | | **19.41** |

**1.9.3b Kiashiria cha ubora wa huduma ya intaneti kwa ukawiaji (ms) kwa maeneo yaliopimwa kwenye robo mwaka iliyoishia Juni 2025**

| Mikoa | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 222 | 61 | 88 | 111 | 57 | 108 |
| Dodoma | 192 | 65 | 82 | 109 | 54 | 100 |
| Katavi | 262 | 101 | 93 | 135 | 125 | 143 |
| Kilimanjaro | 166 | 72 | 65 | 105 | 83 | 98 |
| Manyara | 182 | 62 | 61 | 107 | 60 | 94 |
| Mbeya | 156 | 80 | 106 | 203 | 78 | 124 |
| Mtwara | 168 | 64 | 74 | 109 | 78 | 99 |
| Mwanza | 205 | 76 | 99 | 243 | 74 | 139 |
| Pemba | 214 | 90 | 103 | 259 | 67 | 146 |
| Rukwa | 219 | 81 | 90 | 288 | 63 | 148 |
| Singida | 176 | 109 | 81 | 270 | 50 | 137 |
| Songwe | 182 | 97 | 82 | 200 | 88 | 130 |
| Tabora | 192 | 98 | 95 | 215 | 58 | 132 |
| Unguja | 189 | 69 | 81 | 175 | 52 | 113 |
| **Wastani wa sekta** | | | | | | **122** |

### 1.9.4 Uwezo wa kiunganishi cha intaneti kimataifa

Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje na kuja ndani ya nchi (International Internet link capacity) unakuza matumizi ya Intaneti ndani na nje ya nchi. Jedwali 1.9.4 linaonesha kuwa nchi ina uwezo wa 15,051 Gbps kwa ajili ya uunganishaji wa huduma ya Intaneti. Hii inamaanisha ni asilimia 14.4 pekee ya uwezo wa viunganisho vya kimataifa ambao umetumika.

**Jedwali 1.9.4 Uwezo wa kiunganishi cha huduma ya Intaneti kufikia Juni 2025**

| | Uwezo unaotoka (Gbps) | Uwezo unaoingia (Gbps) |
|---|---|---|
| Jumla ya uwezo uliopo | 17,590 | 17,590 |
| Jumla ya uwezo uliotumika | 2,539 | 2,539 |
| Uwezo unaopatikana kwa uunganishaji mpya | 15,051 | 15,051 |

### 1.9.5 Idadi ya vikoa vya intaneti

Jumla ya idadi ya vikoa vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 33,494 mwishoni mwa Machi 2025 hadi 34,342 mwishoni mwa Juni 2025, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.9.5.

**Jedwali 1.9.5 Idadi ya vikoa vya intaneti**

| Kikoa | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|
| co.tz | 26,196 | 26,905 |
| or.tz | 2,790 | 2,813 |
| ac.tz | 1,173 | 1,194 |
| go.tz | 921 | 931 |
| .tz | 2,085 | 2,170 |
| sc.tz | 273 | 273 |
| ne.tz | 31 | 30 |
| me.tz | 11 | 12 |
| info.tz | 2 | 2 |
| hotel.tz | 2 | 2 |
| mobi.tz | 3 | 3 |
| tv.tz | 3 | 3 |
| mil.tz | 4 | 4 |
| Jumla | 33,494 | 34,342 |


# 1.10 Huduma za Pesa Mtandao

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za pesa mtandao kupitia simu za mkononi zinazotolewa na watoa huduma za pesa mitandao (Mobile Money Operators) kulingana na idadi ya akaunti za pesa mtandao na miamala.

## 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao

Idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kwa asilimia 2 kutoka akaunti milioni 66.5 katika robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025 hadi milioni 68.1 katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025.

**Kielelezo 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao**





**Jedwali 1.10.1 Idadi ya akaunti za pesa mtandao**

| | Aprili | Mei | Juni |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 11,779,914 | 11,656,785 | 11,722,925 |
| Azam Pesa | 37,266 | 42,453 | 38,212 |
| HaloPesa | 5,907,180 | 6,082,865 | 6,249,543 |
| Mixx by Yas | 20,430,998 | 20,839,733 | 20,672,815 |
| T- Pesa | 1,508,952 | 1,369,088 | 1,355,046 |
| M-pesa | 27,396,996 | 27,552,750 | 28,020,749 |
| **Jumla** | **67,061,306** | **67,543,674** | **68,059,290** |

Jedwali 1.10.1 linaonesha kuwa akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 0.7 kwa mwezi katika robo mwaka iliyoishia Juni 2025. Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao imeoneshwa kwenye Chati 1.10.1.

**Chati 1.10.1 Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao**



Chati 1.10.1 inaonesha kuwa soko la pesa mtandao lina ushindani, huku M-pesa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 41.2.

## 1.10.2 Idadi ya miamala ya pesa mtandao

Idadi ya miamala ya pesa mtandao kwa akaunti zilizoweka na kutuma pesa kwa njia ya pesa mtandao katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ya robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.10.2a. Pia, mwenendo wa idadi ya miamala na akaunti kwa robo mwaka na miaka mitano imeoneshwa kwenye jedwali 1.10.2b na 1.10.2c.

### Jedwali 1.10.2a Idadi ya miamala ya pesa mtandao

| | Aprili | Mei | Juni |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 91,968,780 | 99,788,680 | 91,810,220 |
| Azam Pesa | 1,499,761 | 1,496,526 | 1,806,932 |
| HaloPesa | 42,215,295 | 44,253,101 | 42,113,968 |
| T- Pesa | 339,735 | 339,735 | 393,949 |
| M-pesa | 135,531,019 | 141,748,127 | 107604281 |
| Mixx by Yas | 191,439,688 | 200,043,936 | 198,289,442 |
| **Jumla** | **462,994,278** | **487,670,105** | **442,018,792** |

### Jedwali 1.10.2b Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa robo mwaka

| Robo mwaka | Idadi ya akaunti | idadi ya miamala |
|---|---|---|
| Septemba 2024 | 60,815,533 | 879,361,166 |
| Disemba 2024 | 63,207,569 | 1,100,700,205 |
| Machi 2025 | 66,542,276 | 1,366,334,366 |
| Juni 2025 | 68,059,290 | 1,392,683,175 |

### Jedwali 1.10.2c Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa miaka mitano iliyopita

| Mwaka | Idadi ya akaunti | Idadi ya miamala |
|---|---|---|
| 2020 | 32,268,630 | 3,412,210,062 |
| 2021 | 35,285,767 | 3,752,084,894 |
| 2022 | 40,953,496 | 4,195,899,414 |
| 2023 | 52,875,129 | 5,273,086,154 |
| 2024 | 63,207,569 | 3,737,202,434 |

## 1.11 Ubora wa huduma za simu na intaneti


Vipimo vya ubora wa huduma (Quality of Service - QoS) ya simu na Intaneti zinazotolewa na mitandao ya simu nchini vilifanyika kuanzia Aprili hadi Juni 2025 kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma (QoS) na mbinu za vipimo zilizoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025.

### 1.11.1 Upatikanaji wa mtandao

Upatikanaji wa mtandao ni kiashiria kinachoonesha upatikanaji wa mtandao wa simu wakati watumiaji wanataka kutumia huduma za mtandao huo. Lengo ni kufikia zaidi ya 99%.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya maeneo kumi na saba yaliyopimwa. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tano kati ya maeneo kumi na saba yaliyopimwa, Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nne kati ya maeneo kumi na saba na Airtel ilifikia malengo kumi na tatu kati ya malengo kumi na saba kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.1.

**Chati 1.11.1. Upatikanaji wa Mtandao (%) (Lengo ni zaidi ya 99%)**





### 1.11.2 Simu zilizofanikiwa kuunganishwa

Simu zilizofanikiwa kuunganishwa hupimwa kwa asilimia ya simu ambazo ziliweza kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni juu ya 98%.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya maeneo kumi na saba,  Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tano kati ya maeneo kumi na tano kati ya maeneo kumi na sita yaliyopimwa, Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nne kati ya maeneo kumi na saba na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo saba kati ya maeneo kumi na saba yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.2.

**Chati 1.11.2 Simu zilizofanikiwa kuunganishwa**





## 1.11.3 Simu zilizokatika

Kipimo cha kiashiria hiki ni asilimia ya simu zinazokatika kwa sababu za kiufundi kabla ya wahusika kumaliza mazungumzo yao. Lengo ni chini ya 2%.

Halotel na Yas, ilifikia lengo kwenye kwenye sehemu zote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. TTCL na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kwenye maeneo kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na sita ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.3.

**Chati 1.11.3. Matokeo ya Simu zilizokatika**





## 1.11.4 Upatikanaji wa huduma ya 2G

Upatikanaji wa huduma ya 2G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 2G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 2G ni -85 dBm.

Airtel na Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nne kati ya maeneo kumi na saba, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu kati ya maeneo kumi na sita yaliyopimwa, Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na mbili ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.4.

**Chati 1.11.4. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma**





## 1.11.5 Upatikanaji wa huduma ya 3G

Upatikanaji wa huduma ya 3G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 3G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 3G ni -85 dBm.

Airtel, Vodacom, Halotel na Yas zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambayo vipimo vilifanyika. TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na saba kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.5.

**Chati 1.11.5. Matokeo ya kulinganisha upatikanaji wa huduma ya 3G**




## 1.11.6 Upatikanaji wa huduma ya 4G

Upatikanaji wa huduma ya 4G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Lengo la juu kwa teknolojia ya 4G ni -95 dBm.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na saba. Airtel, Halotel na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu kati ya maeneo kumi na nne yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.6.

**Chart 1.11.6. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 4G**





## 1.11.7 Kasi ya kupakua data

Kasi ya kupakua data ni kipimo cha kasi ya uhamishaji data kwenye mtandao. Hupima jinsi data inavyohamishwa haraka kutoka kwa itifaki (protocol) ya uhamishaji faili (File Transfer Protocol - FTP) hadi kwa kifaa cha mawasiliano ya simu. Lengo ni wastani kuwa sawa au zaidi ya 10,000 Kbps.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika, Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya maeneo kumi na saba yaliyopimwa, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne yaliyopimwa na Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili kati ya maeneo kumi na nne kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.7.

**Chati 1.11.7. Matokeo linganishi kwenye kasi ya kupakua data**




## 1.11.8 Muda wa kupata huduma ya data

Muda wa kupata huduma ya data hupimwa kwa muda ambao kifaa cha mtumiaji huchukua kutuma ombi na kupokea jibu kutoka kwenye seva. Lengo ni wastani kuwa chini ya 200ms.

Yas na Vodacom zilifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika, Halotel ilifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo tisa kati ya kumi na nne na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo saba kati ya maeneo kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.8.

**Chati 1.11.8. Matokeo linganishi ya muda wa kupata huduma ya data**





## 1.11.9 Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

Muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inapima muda unaotumika kutoka ujumbe mfupi wa maneno (SMS) inavyotumwa mpaka inapofika kwenye simu husika. Lengo ni chini ya sekunde 2.

Airtel, Vodacom, Yas na Halotel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambapo vipimo vilifanyika. TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tano kati ya kumi na saba yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.9.

**Chati 1.11.9. Matokeo ya muda wa kufika ujumbe mfupi wa maneno**




## 1.11.10 Muda wa kuanzisha simu

Muda wa kuanzisha simu hupimwa kwa muda ambao simu inachukua kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni chini ya sekunde 8.

Halotel, Yas na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na saba ambayo vipimo vilifanyika, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na sita yaliyopimwa na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tano kati ya maeneo kumi na saba kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.10.

**Chart 1.11.10. Matokeo ya kulinganisha muda wa kuanzisha simu**




Matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2025 yanaonesha kuwa Yas ilikuwa na 100%, Halotel 95.0%, Airtel 92.9%, Vodacom ilikuwa na 94.7%, na TTCL 81.3%, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.11.1.

### Jedwali 1.11.1 Matokeo ya ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025

| Mtoa huduma | Kiwango cha ufanisi |
|---|---|
| Yas | 100.0% |
| Halotel | 95.0% |
| Vodacom | 94.7% |
| Airtel | 92.9% |
| TTCL | 81.3% |
| **Wastani wa Sekta** | **92.8%** |

## 1.12 Majaribio ya ulaghai

Jedwali 1.12a linaonesha idadi ya majaribio ya ulaghai kwa kila mkoa kupitia ujumbe wa SMS na sauti.

### Jedwali 1.12a Majaribio ya ulaghai kwa mkoa

| Mkoa | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | | | | | | |
| Rukwa | 362 | 1,544 | 453 | 1,269 | 725 | 4,353 |
| Morogoro | 1,092 | 108 | 968 | 9 | 2,108 | 4,285 |
| Dar es salaam | 538 | 119 | 233 | 26 | 236 | 1,152 |
| Mbeya | 64 | 298 | 148 | 130 | 163 | 803 |
| Kilimanjaro | 24 | 17 | 40 | 0 | 491 | 572 |
| Songwe | 29 | 151 | 63 | 50 | 0 | 293 |
| Katavi | 0 | 117 | 17 | 64 | 72 | 270 |
| Mwanza | 97 | 21 | 53 | 9 | 81 | 261 |
| Iringa | 32 | 169 | 29 | 6 | 11 | 247 |
| Arusha | 69 | 9 | 27 | 17 | 105 | 227 |
| Pwani | 20 | 51 | 39 | 7 | 25 | 142 |
| Dodoma | 26 | 34 | 42 | 18 | 9 | 129 |
| Tabora | 32 | 20 | 19 | 17 | 31 | 119 |
| Kagera | 17 | 12 | 38 | 0 | 44 | 111 |
| Tanga | 14 | 25 | 59 | 3 | 8 | 109 |
| Manyara | 20 | 48 | 9 | 1 | 8 | 86 |
| Geita | 36 | 5 | 25 | 5 | 11 | 82 |
| Ruvuma | 19 | 17 | 32 | 2 | 6 | 76 |
| Shinyanga | 15 | 20 | 9 | 4 | 22 | 70 |
| Mara | 19 | 4 | 15 | 1 | 20 | 59 |
| Kigoma | 11 | 17 | 15 | 1 | 13 | 57 |
| Njombe | 9 | 21 | 16 | 2 | 9 | 57 |
| Mtwara | 12 | 9 | 17 | 8 | 6 | 52 |
| Singida | 6 | 12 | 12 | 4 | 9 | 43 |
| Lindi | 5 | 12 | 15 | 4 | 2 | 38 |
| Simiyu | 11 | 14 | 9 | 1 | 3 | 38 |
| **Zanzibar** | | | | | | |
| Mjini Magharibi | 16 | 4 | 24 | 0 | 6 | 50 |
| Kusini Pemba | 0 | 2 | 16 | 0 | 0 | 18 |
| Kaskazini Unguja | 0 | 0 | 17 | 0 | 0 | 17 |
| Kaskazini Pemba | 0 | 2 | 11 | 0 | 0 | 13 |
| Kusini Unguja | 0 | 0 | 8 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | **2,595** | **2,882** | **2,478** | **1,658** | **4,224** | **13,837** |


Kielelezo hapo chini kinaonesha majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma kwa robo ya mwaka inayoishia Machi 2025 na Juni 2025. Vodacom ilikuwa na idadi ya majaribio mengi zaidi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, aidha TTCL ilikua na majaribio machache ikilinganishwa na watoa huduma wengine.

### Jedwali 1.12b Majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma

| Robo ya mwaka inayoishia | Airtel | Halotel | Yas | TTCL | Vodacom | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Machi 2025 | 5,876 | 1,724 | 2,484 | 3,925 | 3,143 | 17,152 |
| Juni 2025 | 2,595 | 2,882 | 2,478 | 1,658 | 4,224 | 13,837 |
| Badiliko | -56% | 67% | -0.2% | -58% | 34% | -19% |

Takwimu zinaonesha kuwa majaribio ya ulaghai kwa ujumla yamepungua kwa wastani wa 19%. Chati 1.12a inaonesha majaribio ya ulaghai kimkoa. Mikoa ya Rukwa na Morogoro ndiyo inayoongoza kwa majaribio ya ulaghai nchini.

### Chati 1.12a Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Juni 2025




### Jedwali 1.12c Majaribio ya ulaghai kiwilaya kwa mikoa minne inayoongoza

| Region | District | Fraudulent attempts |
|---|---|---|
| Rukwa | Kalambo | 617 |
| | Nkasi | 915 |
| | Sumbawanga Rural | 1,536 |
| | Sumbawanga Urban | 1,285 |
| | | |
| Morogoro | Gairo | 8 |
| | Kilombero | 3,955 |
| | Kilosa | 44 |
| | Morogoro Rural | 70 |
| | Morogoro Urban | 16 |
| | Mvomero | 13 |
| | Ulanga | 102 |
| | Malinyi DC | 40 |
| | Mlimba DC | 37 |
| | | |
| Dar es Salaam | Ilala | 230 |
| | Kigamboni | 28 |
| | Kinondoni | 357 |
| | Temeke | 238 |
| | Ubungo | 299 |
| | | |
| Mbeya | Chunya | 105 |
| | Kyela | 22 |
| | Mbarali | 57 |
| | Mbeya vijijini | 323 |
| | Mbeya mjini | 242 |
| | Rungwe | 54 |
| | | |

**Chati 1.12b Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma**

Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma imeoneshwa katika Chati 1.12b.




## 1.13 Leseni za huduma ya Mawasiliano ya simu na intaneti

| Mawasiliano ya simu na Intaneti | | |
|---|---|---|
| **Aina ya leseni** | **Idadi ya leseni** | |
| | **Machi 2025** | **Juni 2025** |
| Network Facilities Licences | 44 | 44 |
| Network Services Licences | 18 | 19 |
| Application Services Licences | 144 | 150 |
| Aircraft Stations | 187 | 163 |
| Amateur Stations | 20 | 18 |
| Fixed VSAT Terminals | 37 | 26 |
| Mobile VSAT Terminals | 2 | 2 |
| Satellite Ground Earth Stations | 1 | 1 |
| Ship Stations | 30 | 30 |
| HF Radio Stations | 19 | 16 |
| VHF- UHF Radio Repeaters | 2 | 1 |
| VHF - UHF Radio Station with Pair of Frequency | 109 | 113 |
| VHF - UHF Radio Station with Single Frequency | 182 | 183 |
| Numbering | 529 | 187 |

## 1.14 Vyeti

| Aina ya cheti na idadi | | |
|---|---|---|
| **Aina ya cheti** | **Idadi ya vyeti** | |
| | **Machi 2025** | **Juni 2025** |
| Global Maritime Distress and Safety Systems | 231 | 245 |
| Type Approval | 5,120 | 5,253 |
| Registration for Satellite Mobile Phones | 46 | 46 |

# Sura ya pili

## Huduma za Utangazaji



# 2. Huduma za Utangazaji


Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), setelaiti (DTH), na kwa njia ya waya (Cable TV), pamoja na maeneo ya kijografia na idadi ya watu waliofikiwa na mawimbi ya huduma za utangazaji. Pia inatoa tathmini wa uzingatiaji wa ubora wa huduma.

## 2.1 Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ili kupata huduma za utangazaji za televisheni imepungua kwa asilimia 1.1 kama invyooneshwa kwenye kielelezo hapo chini.

| Kufikia Machi 2025 | Kufikia Juni 2025 | |
|---|---|---|
| **Milioni 2.1** | **Milioni 2.0** | **1.1%** |

**Kielelezo 2.0 Mgawanyiko wa visimbuzi vilivyolipiwa**




Kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025, Azam Media Limited ilikua na idadi kubwa ya visimbuzi ikifuatiwa na Star Media Limited kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 2.1.


**Jedwali 2.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu**

| Mtoa huduma | Visimbuzi vya DTT | Visimbuzi vya DTH | Jumla ya visimbuzi vilivyolipiwa |
|---|---|---|---|
| Azam Media Limited | 296,385 | 1,048,367 | 1,344,752 |
| Basic Transmissions Limited (Continental) | 35,063 | 28,810 | 63,873 |
| Multichoice Tanzania Limited (DStv) | 0 | 189,272 | 189,272 |
| Star Media Limited | 203,640 | 213,978 | 417,618 |
| Zuku | 0 | 19,804 | 19,804 |
| **Jumla** | **535,088** | **1,500,231** | **2,035,319** |

Agape Associates Limited na Basic Transmissions Limited (Digitek) hawakuwa na visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu.

Ramani 2.1 inaonesha idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa. Dar es Salaam ina visimbuzi vingi (662,368), ikifuatiwa na Mwanza (169,550), Mbeya (136,899), Arusha (125,390) na mikoa mingine ni kama ilivyooneshwa kwenye ramani.

**Ramani 2.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa**




## 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya (Cable TV subscriptions) zimeongezeka kwa 3% kutoka 17,185 kwa robo mwaka inayoishia Machi 2025 na kufikia 17,657 katika kipindi cha robo mwaka inayoishia Juni 2025.


**Kielelezo 2. 2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya**

| Kufikia Machi 2025 | Kufikia Juni 2025 |
|---|---|
| 17,185 | 17,657 |

3%

Idadi ya televisheni kwa kila mkoa katika kipindi husika imeoneshwa kwenye Chati 2.2.

**Chati 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kufikia Juni 2025**




Kwa mikoa yote Tanzania Bara, Shinyanga inaongoza kwa kuwa na televisheni nyingi zinazopokea maudhui kwa njia ya waya (4,370), ikifuatiwa na Mwanza (1,990), Tabora (1,809), na Arusha (1,440). Mikoa yenye televisheni chache kwa njia ya waya ni Katavi (43), Iringa (99) na Ruvuma (127).

Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya zimeoneshwa kwenye Jedwali 2.2a na 2.2b.

**Jedwali 2.2a Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa robo mwaka**

| | Septemba 2024 | Disemba 2024 | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Usajili | 19,153 | 16,767 | 17,185 | 17,657 |

**Jedwali 2.2b Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Usajili | 14,350 | 19,739 | 22,295 | 16,223 | 16,767 |

## 2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji

Takwimu zinaonesha kuna utofauti wa ueneaji wa huduma za utangazaji kwa njia ya DTT, DTH na redio ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali 2.3.

**Jedwali 2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji hadi kufikia Juni 2025**

| Kiashiria | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|
| % ya watu waliofikiwa na mawimbi na DTT | 58.00% | 58.00% |
| % ya watu waliofikiwa mawimbi na DTH | 100.00% | 100.00% |
| % ya watu waliofikiwa na mawimbi ya redio za FM | 81.45 | 83.40% |
| % ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTT | 33.00% | 33.00% |
| % ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTH | 100.00% | 100.00% |
| % ya eneo lililofikiwa na mawimbi redio za FM | 56.95% | 58.30% |

## 2.4 Utekelezaji wa masharti ya leseni za utangazaji

Ufuatiliaji wa maudhui kwa watoa huduma za utangazaji wa kitaifa nchini ulifanyika kuanzia Aprili hadi Juni 2025 kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma na vipimo vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2025.

### 2.4.1 Uwasilishaji na uzingatiaji wa ratiba ya vipindi

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuwasilisha ratiba ya vipindi ikionesha muda, mpangilio, na idadi, na kuzingatia ratiba ya vipindi wanavyokusudia kurusha hewani. Uzingatiaji wa uwasilishaji wa mpangilio wa vipindi na kufuata ratiba kwa robo mwaka iliyotathminiwa umeonyeshwa kwenye Jedwali 2.4.1a na 2.4.1b.

**Jedwali 2.4.1a  Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya televisheni**

| TV | Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi | Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi |
|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Imekidhi |
| UTV | Imekidhi | Imekidhi |
| Tumaini TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Haijakidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Haijakidhi | Haijakidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Imekidhi |
| WRM TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Imekidhi |
| Hope Channel Tanzania | Imekidhi | Imekidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Haijakidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Haijakidhi |
| TVE | Imekidhi | Imekidhi |

### Jedwali 2.4.1b Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya redio

| Redio | Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi | Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi |
|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Haijakidhi |
| Clouds FM | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi |
| EFM | Imekidhi | Haijakidhi |
| Wasafi FM | Imekidhi | Imekidhi |
| Magic FM | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Haijakidhi | Haijakidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Haijakidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi |

## 2.4.2 Utofauti wa vipindi, maudhui ya elimu na uzingatiaji wa dakika tisini ya utoaji wa habari

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kutoa maudhui anuai ili kukidhi tamaduni na mahitaji ya rika tofauti. Pia wanatakiwa kutoa maudhui ya elimu na kutenga muda wa dakika tisini kwa ajili wa habari na matukio. Uzingatiaji wa uanuai wa vipindi kwa robo mwaka

### Jedwali 2.4.2a Uanuai wa vipindi vya televisheni

| TV | Utofauti wa vipindi | Maudhui ya elimu | Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari |
|---|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| UTV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Tumaini TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| WRM TV | Haijakidhi | Haijakidhi | Imekidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Hope Channel Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| TVE | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

**Jedwali 2.4.2b Uanuai wa vipindi vya redio**

| Redio | Utofauti wa vipindi | Maudhui ya elimu | Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari |
|---|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| Clouds FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| EFM | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| Wasafi FM | Imekidhi | Imekidhi | Haijakidhi |
| Magic FM | Haijakidhi | Haijakidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

## 2.4.3 Uzingatiaji wa maudhui ya ndani (local content)

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya vipindi vyao vimetengenezwa ndani ya nchi, ili kuchagiza utamaduni, lugha, na maudhui ya ndani ya nchi. Matokeo ya upimaji ya uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwa robo mwaka yameoneshwa kwenye Jedwali 2.4.3a na Jedwali 2.4.3b.

**Jedwali 2.4.3a Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni**

| TV | Yenye manufaa kwa jamii | Lugha (Kiswahili au Kiingereza) | 60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani |
|---|---|---|---|
| ITV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| UTV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Tumaini TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Television | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Star TV Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC 1 | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TV Imaan | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Arise and Shine TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| WRM TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Hope Channel Tanzania | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Upendo TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Mahaasin TV | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Channel Ten Plus | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TVE | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

### Jedwali 2.4.3b Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio

| Redio | Yenye manufaa kwa jamii | Lugha (Kiswahili au Kiingereza) | 60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani |
|---|---|---|---|
| Radio One | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC Taifa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Adventist World Radio (AWR) | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Clouds FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| East Africa Radio | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| EFM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Wasafi FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Magic FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| TBC International | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Free Africa | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Bongo FM | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |
| Radio Maria | Imekidhi | Imekidhi | Imekidhi |

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

## 2.5 Leseni za huduma za Utangazaji

| Aina ya leseni | Idadi ya leseni | |
|---|---|---|
| | Machi 2025 | Juni 2025 |
| National Content Television (FTA) Licences | 17 | 17 |
| District Content Television (FTA) Licences | 21 | 21 |
| National Content Radio Licences | 14 | 14 |
| Regional Content Radio Licences | 33 | 36 |
| District Content Radio Licences | 187 | 184 |
| Community Radios | 17 | 17 |
| National Content Televisions by Subscription | 30 | 30 |
| District Content Televisions by Subscription | 1 | 1 |
| National Content ( support services) | 3 | 3 |
| Online Content Aggregators | 6 | 6 |
| Weblogs (Blogs) | 64 | 72 |
| Online Radios | 10 | 11 |
| Online Televisions | 196 | 213 |
| Cable Televisions | 50 | 56 |

# Sura ya tatu

## Huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto



# 3. Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto

Sehemu hii inawasilisha takwimu za masanduku ya posta, wateja, huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, zilizotumwa na kupokelewa, kwenda na kutoka ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

## 3.1 Idadi ya masanduku ya posta

Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatoa huduma za msingi za posta za masanduku na mifuko binafsi ya barua kwa watu binafsi na kampuni. Idadi ya masanduku na mifuko binafsi katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2025, ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1 Masanduku na mifuko binafsi ya barua**

| Mwezi | Masanduku ya barua | Mifuko binafsi ya barua | Jumla |
|---|---|---|---|
| Aprili | 158,006 | 67 | **158,073** |
| Mei | 158,006 | 67 | **158,073** |
| Juni | 158,006 | 67 | **158,073** |

## 3.2 Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2025 imeoneshwa kwenye Jedwali 3.2.

**Jedwali 3.2 Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi/vipeto**

| Mwezi | Kampuni/Taasisi | Wateja binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|
| Aprili | 1,661 | 89,235 | **90,896** |
| Mei | 3,948 | 51,407 | **55,355** |
| Juni | 1,042 | 63,972 | **65,014** |

Jedwali 3.2 inaonesha kuwa wateja binafsi ni wengi zaidi kuliko wateja wa makampuni/taasisi.

## 3.3 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa

### 3.3.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi


Takwimu zinaonesha Nyaraka (Document) zilitumwa zaidi katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Juni 2025, ikifuatiwa na Vifurushi (Parcels). Mizigo (Cargo) vimetumwa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi hicho. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa katika kipindi husika zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.3.

**Jedwali 3.3.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Juni 2025**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 55,796 | 84,297 | 5,862 | 48,648 | 15,471 | 210,074 |
| Mei | 49,320 | 60,091 | 6,998 | 52,407 | 8,879 | 177,695 |
| Juni | 49,489 | 60,968 | 7,537 | 50,363 | 3,400 | 171,757 |
| Jumla | 154,605 | 205,356 | 20,397 | 151,418 | 27,750 | 559,526 |

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na TPC na watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji ndani ya nchi ilikua ni 281,099 kwa watoa huduma binafsi na 278,427 kwa TPC. Watoa huduma binafsi ikiwa na idadi kubwa zaidi (50.2%) ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi ikilinganishwa TPC (49.8%) kama ilivoneshwa katika Chati 3.3.

**Chati 3.3 Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi**




## 3.3.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kupitia TPC na watoa huduma wengine wa huduma ya usafirishaji katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 3.3.2a.

**Jedwali 3.3.2a Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kwa mtoa huduma**

| Watoa huduma | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|
| TPC | 41,966 | 36,096 |
| Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 25,495 | 25,506 |
| Jumla | 67,461 | 61,602 |

Jedwali 3.4b linaonesha idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa barua zimetumwa zaidi nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Juni 2025, ikifuatiwa na vifurushi.

**Jedwali 3.3.2b Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 9,667 | 5,811 | 186 | 3,732 | 17 | 19,413 |
| Mei | 8,675 | 5,907 | 261 | 4,372 | 4 | 19,219 |
| Juni | 14,312 | 4,233 | 136 | 4,285 | 4 | 22,970 |
| Jumla | 32,654 | 15,951 | 583 | 12,389 | 25 | 61,602 |

## 3.4 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa

### 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kupitia TPC na watoa huduma wengine wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto imeoneshwa kwenye jedwali 3.4.1.

**Jedwali 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa ndani ya nchi kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 209,695 | 73,098 | 4,609 | 38,767 | 14,642 | 340,811 |
| Mei | 171,679 | 51,519 | 6,879 | 58,558 | 8,326 | 296,961 |
| Juni | 212,325 | 52,210 | 6,776 | 42,492 | 3,15 | 316,960 |
| Jumla | 593,699 | 176,827 | 18,264 | 139,817 | 26,125 | 954,732 |

### 3.4.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2025 imeoneshwa kwenye jedwali 3.4.2a.

**Jedwali 3.4.2a Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa watoa huduma**

| Watoa huduma | Machi 2025 | Juni 2025 |
|---|---|---|
| TPC | 66,989 | 56,001 |
| Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto | 52,465 | 20,783 |
| Jumla | 119,454 | 76,784 |


Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.4.2b. Barua kutoka nje ya nchi zimepokelewa kwa idadi kubwa zaidi ikilinganisha na bidhaa nyingine katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025, wakati mizigo kutoka nje ya nchi ilipokelewa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi husika.

**Jedwali 3.4.2b Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa aina ya huduma**

| Mwezi | Barua | Vifurushi | Vipeto | Nyaraka | Mizigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aprili | 8,501 | 5,492 | 8,333 | 6,965 | 26 | 29,317 |
| Mei | 6,699 | 6,857 | 9,369 | 2,073 | 25 | 25,023 |
| Juni | 12,107 | 1,559 | 7,757 | 1,006 | 15 | 22,444 |
| Jumla | 27,307 | 13,908 | 25,459 | 10,044 | 66 | 76,784 |

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na kupokelewa unaonesha kuwa Tanzania ilituma bidhaa za kiposta chache zaidi nje ya nchi (45%) kuliko ilivyopokea (55%) kama ilivyooneshwa kwenye Chati 3.4.

### Chati 3.4 Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi




## 3.5 Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Juni 2025, vipimo vya Ubora wa Huduma (QoS) vilifanyika katika kanda A, B na C ili kutathmini jinsi huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto zilivyokidhi viwango vya utoaji huduma vilivyowekwa kwenye kanuni za ubora.

Kanda A (Inter-Town Zone A) inayojumuisha miji ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Iringa, Zanzibar na Mwanza kiwango kinahitaji 90% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1). Kanda B (Inter-Town Zone B), inayojumuisha miji ya Mbeya, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Singida na Lindi, na Kanda C (Inter-Town Zone C) inayojumuisha miji ya Tabora na Geita ambapo kote kiwango kinahitaji 90% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku mbili (D+2). Matokeo ya upimaji yameoneshwa kwenye jedwali 3.5a na 3.5b.

### Jedwali 3.5a Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda A (90% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1)

| Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi | Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda A |
|---|---|
| Advanced Logistics Limited | Haijakidhi |
| Couriemate Tanzania Limited | Haijakidhi |
| H&N Courier Express Limited | Haijakidhi |
| Cmtl Group Limited | Haijakidhi |
| Marathon Logistics Limited | Haijakidhi |
| Ab Courier Express Limited | Imekidhi |
| Blaze Concierge And Courier Services Limited | Imekidhi |
| Mwananchi Communications Limited | Imekidhi |
| Geamos Company Limited | Imekidhi |
| Air Tanzania Company Limited | Imekidhi |
| Madeira Courier Services | Imekidhi |
| Ndengaro Company Limited | Imekidhi |
| Precision Air Services Plc | Imekidhi |
| Zan Fast Ferries Company Limited | Imekidhi |

**Jedwali 3.5a Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda B na C (90% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku mbili (D+2)**

| Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi | Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda B na C (D+2(90%)) |
|---|---|
| Simba Logistic Equipment Supply Co. Ltd | Haijakidhi |
| Couriemate Tanzania Limited | Haijakidhi |
| H&N Courier Express Limited | Haijakidhi |
| Cmtl Group Limited | Haijakidhi |
| Advanced Logistics Limited | Haijakidhi |
| Ndengaro Company Limited | Haijakidhi |
| Mwananchi Communications Limited | Imekidhi |
| Marathon Logistics Limited | Imekidhi |
| Ab Courier Express Limited | Imekidhi |
| Blaze Concierge And Courier Services Limited | Imekidhi |
| Geamos Company Limited | Imekidhi |
| Air Tanzania Company Limited | Imekidhi |
| Precision Air Services Plc | Imekidhi |
| Malitabu Musa Ntamala T/A Skygo Express | Imekidhi |

TCRA imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

## 3.6 Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto

| Aina ya leseni | Idadi | |
|---|---|---|
| | **Machi 2025** | **Juni 2025** |
| International Courier | 5 | 6 |
| East Africa Courier | 2 | - |
| Intercity Transporters | 79 | 71 |
| Intracity Courier | 15 | 13 |
| Domestic Courier | 49 | 55 |
| Public Postal | 1 | 1 |

# 4. Hitimisho

Sekta ya mawasiliano imeonesha ukuaji endelevu katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2025. Sekta ndogo zote tatu za mawasiliano ya simu na intaneti, huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, pamoja na utangazaji ziliendelea kukua katika utoaji wa huduma na ushindani wa kibiashara.

Katika huduma za mawasiliano ya simu na intaneti, kumekuwa na ongezeko katika idadi ya usajili, utumiaji, na upatikanaji wa huduma. Hata hivyo, gharama za huduma za sauti, data, na ujumbe mfupi wa maneno (SMS) hazikua na mabadiliko makubwa. Soko hili limeendelea kuwa na ushindani mkubwa, ambapo kampuni tatu za mawasiliano ya simu zinashikilia kwa pamoja asilimia 82.6 ya soko, huku hakuna kampuni iliyozidi kiwango cha umiliki mkubwa wa asilimia 35. Usajili wa intaneti na matumizi yake umeongezeka kwa asilimia 9.6 na asilimia 14.7 mtawalia, kutokana na kuenea kwa intaneti ya kasi kupitia teknolojia ya 4G na 5G nchini kote, sambamba na ongezeko la watu na maeneo yaliyofikiwa na huduma.

Huduma za utangazaji zinazopimwa kupitia idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa, hazikubadilika ikilinganishwa na robo ya mwaka iliyopita. Hata hivyo, kumekuwa na mabadiliko katika uchaguzi wa watumiaji, huku idadi ya waliojisajili kwenye televisheni ya setelaite (DTH) ikiongezeka kutokana na kuenea nchi nzima kwa asilimia 100, na kushuka kwa idadi ya watumiaji wa televisheni inayotumiwa miundombinu iliyosimikwa ardhini (DTT), ambayo imefikia asilimia 33 kijiografia na asilimia 58 ya watu. Soko la utangazaji limeendelea kuwa na nguvu na kuvutia watoa huduma wapya, hususan kwenye huduma za televisheni za mtandaoni, blogu, na televisheni kwa njia ya waya. Sekta hii ilipokea watoa huduma wapya 32, sawa na ongezeko la asilimia 5, na kufikisha jumla ya watoa huduma 681.

Shirika la Posta Tanzania pamoja na wasafirishaji wa vifurushi na vipeto wameendelea kuwa na mchango mkubwa katika sekta hii kwa kuwezesha upokeaji na usambazaji wa barua, vifurushi, nyaraka na mizigo. Hali hii imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza biashara ya mtandaoni na uchumi wa kidijitali kwa ujumla. Ufanisi wa huduma hizi unatarajiwa kuimarika zaidi kufuatia maboresho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za mwaka 2024, ambazo zimeondoa mipaka ya kijiografia kwenye soko la posta la ndani, hivyo kuwezesha watoa huduma kukuza huduma katika maeneo yenye kuvutia kibiashara.

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania